# <JINA LA KIJIJI>

## Mpango wa usimamizi moto

## <jina la msitu>

**<kuanzia tarehe> – <hadi tarehe>**

# 1: UTANGULIZI

Kabrasha hili litatumika pamoja na mpango wa usimamizi Misitu na Sheria ndogo za Kijiji zilizoandaliwa na kamati ya maliasili ya kijiji cha <Jina la Kijiji> chini ya uwezeshaji wa Shirika la kuhifadhi mpingo na maendeleo. Sheria ndogo za kijiji zilipitishwa na Baraza kuu la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa <tarehe>.

Kabrasha hili linatoa mwongozo wa usimamizi wa moto katika msitu wa<Jina la Msitu>

Njia kuu ya usimamizi moto katika msitu itakuwa ni ubabuaji. Ubabuaji utatumika kuzuia moto unaoingia msituni pamoja na kupunguza hatari ya mioto mikali ndani ya msitu. Ubabuaji utafanyika kwa njia nne kama ifuatavyo:

1. Ubabuaji wa moto kuzuia katika mipaka ya msitu.
2. Ubabuaji kando ya barabara na njia zinazopita katika msitu.
3. Ubabuaji wa kupunguza hatari za moto katika maeneo ambayo mioto huingilia.
4. Ubabuaji ndani ya msitu ili kupunguza mrundikano wa majani makavu ambayo huweza kusababisha mioto mikubwa na miharibifu.

Mpango wa ubabuaji unakabiliwa na changamoto ya jinsi ardhi ya msitu ilivyo, Ili kujua ni maeneo gani ya kubabua na kwa muda gani itategemea na namna msitu ulivyo (Miinuko na mabonde katika msitu). Shughuli zote za ubabuaji ni lazima zifanyike kwa makini na uangalizi wa hali ya juu na kwa kipindi kisichozidi miezi miwili baada ya mvua za masika kumalizika.

# 2: MAENEO HATARISHI KWA MIOTO

Kiambatisho na 1. kinaonesha ramani ya msitu pamoja na maeneo hatarishi kwa moto, maeneo hayo ni kama yafuatayo:-

- Msitu una mpaka wenye urefu unaokadiriwa kuwa kilomita XX.
- Makisio ya barabara na njia zinazokatisha msitu ni kmXX. Za muhimu zaidi ni:
  - Barabara kutoka A kwenda B (Kilomita...)
  - Njia za miguu kutoka C kwenda D (Kilomita)

- Upepo kipindi cha kiangazi huvuma kutoka mashariki hivyo mioto mingi huingia msituni kutoka pande hizo. Hususani mioto huingilia toka sehemu zifuatazo:
  - Kutoka kilima kilichopo upande wa....
  - Upande wa bonde liitwalo.....
  - ...
- Maeneo ndani ya msitu ambayo yako hatarini kuathirika na mioto ni.........., kwa sababu ni..........
- Vizuizi vya asili vya mioto ndani ya msitu vipo katika maeneo yafuatayo.............

Ili kukabili mioto katika maeneo haya ubauaji wa ziada zaidi ya ule wa mipaka utahitajika kufanyika katika maeneo yafuatayo......na kwa njia ya...........

## 3: KASI YA UKAUKAJI

Kuna kipindi kifupi sana katika mwaka ambacho ubabuaji unaweza kufanywa kwa ufasaha. Kabla ya kipindi hiki nyasi huwa mbichi sana kwa ubabuaji na baada ya kipindi hiki nyasi huwa kavu sana kwa ubabuaji kufanyika kwa usalama. Hata hivyo msitu wote huwa haukauki kwa kiwango sawa katika kipindi hiki baada ya mvua, hivyo basi kipindi hiki kifupi hutofautiana katika sehemu tofauti za msitu. Maeneo ya msitu ambayo hukauka mapema ni:

- Fafanua maeneo ambayo hukauka mapema
- ...

Maeneo ya msitu ambayo hukauka kwa kuchelewa ni:

- Elezea maeneo ambayo hukauka kwa kuchelewa
- ...

Baadhi ya maeneo ya msitu huwa hayakauki mwaka mzima, maeneo haya hayatakiwi kuchomwa kwa ubabuaji kamwe. Maeneo haya ni:

- Elezea maeneo yasiyokauka mwaka mzima
- ...

## 4: TARATIBU ZA UBABUAJI

Taratibu zifuatazo zitafuatwa kipindi ubabuaji utakapofanyika.

### Maandalizi kabla ya ubabuaji

- Kabla ubabuaji haujafanyika wanajamii wa kijiji hiki cha ......na wa vijiji vya ......jirani watafahamishwa juu ya zoezi la ubabuaji.
- Timu ya wababuaji itaundwa na itakuwa na wataalamu wawili na wanajamii 6-15; Watu wenye matatizo ya pumu na matatizo mengine kiafya hawataruhusiwa kushiriki zoezi hili la ubabuaji.
- Watu wote katika timu ya ubabuaji watakubaliana jukumu la kila mmoja wao ili kuzuia moto kuwatoroka na kuumizana kati yao.
- Mioto itawashwa na kusimamiwa kwa kutumia zana maalumu za mikono.
- Vitu maalum vya kuzimia moto kama vile mafukutu, panga, chepeo na vingine vinatakiwa kuwepo katika eneo la ubabuaji kabla ya zoezi kuanza.

### Aina za ubabuaji

- Mipaka ya msitu, kingo za barabara na njia za miguu vyote zitababuliwa angalau upna wa mita 100 kwa kila upande ili kupunguza hatari ya mioto kuvuka kipindi cha upepo mkali.
- Maeneo mengine yaliyopo mbali na mipaka na barabara, ndani ya msitu yatababuliwa kwa maeneo tofauti tofauti kutegemeana na hali ya eneo la msitu kama ilivyoainishwa katika ramani ya msitu hapo chini.
- Ili kuhakikisha maeneo tofauti yanababuliwa mara kwa mara , maeneo yatababuliwa kwa kila kipindi cha kisichopungua miaka miwili.

### Shughuli ya ubabuaji

- Ubabuaji utafanyika wakati wa asubuhi tu pindi ukungu unapotoweka. Hakuna mioto itakayowashwa baada ya saa tano asubuhi.

- Ubabuaji hautafanyika endapo kutakuwepo na upepo mkali ambao utazuia kuthibiti moto.
- Mioto midogo ambayo itasambaa vizuri na kuweza kudhibitiwa ndio itakayowashwa.
- Ubabuaji utafanyika kwa kutumia mioto itakayo washwa kukingana na mwelekeo wa upepo.
- Katika maeneo ambayo hakuna kinga za moto za asili au maeneo yaliyokwisha ungua mwanzo, kinga ndogondogo za moto zitatengenezwa ili kuzuia moto kusambaa. Miti yoyote iliyozidi kipimo DBH ya sintimeta 5 haitakatwa katika kutengeneza vizuizi hivi vya mioto.

## Baada ya ubabuaji

Lazima kuweka kumbukumbu za ubabuaji kwa kila siku kwa kuzingatia yafuatayo:

- Wapi (eneo) lililobabuliwa
- Hali ya hewa katika kipindi cha ubabuaji
- Washiriki katika zoezi la ubabuaji
- Matatizo yaliyojitokeza katika shughuli ya ubabuaji

# 5: RATIBA YA UBABUAJI

Jedwali hapo chini linaonyesha lini kila eneo la msitu litafanyiwa ubabuaji. Muda wa ubabuaji umewekwa kwa makisio (Umekadiriwa). Ili kujua wakati muafaka wa ubabuaji, maeneo yanayokauka haraka (ambayo ni.......) katika msitu yatakaguliwa kila wiki baada ya msimu wa mvua kumalizikaa. Pindi maeneo haya yanapokuwa makavu na tayari kwa kufanyiwa ubabuaji basi ratiba ya ubabuaji itaanza na kutekelezwa katika muda wa kila wiki kama inavyoonyeshwa hapo chini.

| Muda baada ya Mvua kwisha | Shughuli za Ubabuaji |
|---|---|
| Wiki ya 5 | Katika mipaka na njia zipi?<br>Ubabuaji katika maeneo tofauti ndani ya msitu (Yatajwe)<br>Ubabuaji wa ziada katika maeneo gani hatarishi ya moto? |
| Wiki ya 6 | Katika mipaka na njia zipi?<br>Ubabuaji katika maeneo tofauti ndani ya msitu (Yatajwe)<br>Ubabuaji wa ziada katika maeneo gani hatarishi ya moto? |
| Wiki ya 7 | Katika mipaka na njia zipi?<br>Ubabuaji katika maeneo tofauti ndani ya msitu (Yatajwe)<br>Ubabuaji wa ziada katika maeneo gani hatarishi ya moto? |
| Wiki ya 8 | Katika mipaka na njia zipi?<br>Ubabuaji katika maeneo tofauti ndani ya msitu (Yatajwe)<br>Ubabuaji wa ziada katika maeneo gani hatarishi ya moto? |
| Wiki ya 9 | Katika mipaka na njia zipi?<br>Ubabuaji katika maeneo tofauti ndani ya msitu (Yatajwe)<br>Ubabuaji wa ziada katika maeneo gani hatarishi ya moto? |

## KIAMBATISHO I : RAMANI SHIRIKISHI YA MSITU KWA AJILI YA USIMAMIZI WA MOTO